**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA ROMBO**
**SHULE YA SEKONDARI KENI**

**SHULE YA SEKONDARI KENI,**
S. L. P 144,
**MKUU- ROMBO.**
08/07/2024.

SIMU: KWA MAWASILIANO.
i) 0755- 642415 Mkuu wa shule.
ii)0768-651099/ 0627052935/0622109659- M/Mkuu wa Shule.
iii) 0769-740284/0627-780038 Mtaaluma
iv)0759-172854/0694105630. Matron /mlezi wa wasichana.
v)0747-590773.patron/mlezi wa wavulana.

Mzazi / Mlezi / Mfadhili wa Mwanafunzi……………………………………………………

YAH: **MAAGIZO YA KUJIUNGA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI KENI MWAKA 2024 / 2025.**

## A. UTANGULIZI

Kwa niaba ya Jumuiya ya Shule ya Sekondari Keni iliyoko Wilaya ya Rombo Mkoa wa Kilimanjaro, ninayo furaha kukujulisha kwamba mwanao aliyekuwa akisoma Shule ya Sekondari…………………………………. amechaguliwa kujiunga katika **Shule ya Sekondari Keni** kidato cha Tano tahasusi ya EGM kwa mwaka huu wa 2024 / 2025. Shule itafunguliwa tarehe ……………. na mwanao afike Siku hiyo shuleni ili aweze kusajiliwa.

Shule ya Sekondari Keni ni Shule nzuri ya wanafunzi kuanzia kidato cha I -VI. Shule ya Sekondari Keni iko katika mazingira mazuri ya mwanafunzi kusoma na kuweza kufaulu vizuri kama ataonyesha bidii ya kusoma. Shule inayo walimu wa kutosha na huduma zote muhimu kwa wanafunzi zinapatikana shuleni. Mwanao aitumie nafasi hii aliyopewa na Serikali ili baadaye alisaidie Taifa letu, wazazi wake na yeye mwenyewe.

***Tunakupongeza wewe mzazi pamoja na mwanao kwa kupata nafasi hii.***

## B. USAFIRI WA KUFIKA SHULENI

Mwanafunzi akifika Moshi Mjini kituo kikuu cha mabasi akitokea popote pale, aulize na kupanda magari yaendayo Rombo- Mkuu. Shule yetu ipo umbali wa kilometa 54 kutoka Moshi Mjini Nauli ya kutoka Moshi Mjini hadi Mkuu Rombo ni Tshs. 3000 hadi Tshs 4000 kutegemea na aina gari. Kwa wanafunzi wanaotoka Dar es Salaam au kupitia Dar es Salaam wapande magari ya *Dar express, Tilisho, Esther luxury* yanayokuja moja kwa moja Rombo. Kwa wanaotoka Dodoma wapande *Shabiby* na kwa wanaotoka Mikoa na mingine wapande mabasi yanayofika hadi Moshi Mjini na kisha kupanda usafiri mwingine hadi shuleni.

## C. KITUO CHA KUTEREMKIA

Ukitokea, Dar es Salaam, Dodoma na Moshi mjini mwambie kondakta wa gari utateremkia kituo cha afya- Keni. Vilevile kwa wale wanaotokea Tarakea nao watateremkia kituo cha cha afya –Keni. Kutoka kituo cha magari cha kushukia (kituo cha afya Keni) kuelekea shuleni ni umbali wa mita 50 utakuwa umefika shuleni. Ukifika shuleni utaripoti na kupokelewa na mwalimu wa zamu au Makamu

wa Mkuu wa shule ambao wote watakuwepo shuleni kwa kipindi hicho (Kuanzia Saa moja Asbh hadi Saa moja Usiku) . Baada ya kuripoti shuleni utasajiliwa ofisini kwa makamu wa mkuu wa shule ukiwa na mahitaji yote muhimu uliyoagizwa kuleta shuleni.

**D. HUDUMA ZINAZOPATIKANA SHULENI**

Shule ina duka ambalo hutoa huduma na mahitaji karibu yote muhimu kwa wanafunzi na watumishi wote wa shule. Kituo cha afya Keni kipo karibu na shule. Hospitali kubwa ya Wilaya ipo karibu na shule, usafiri wa kuja shuleni na kurudi nyumbani ni mzuri kwani shule ipo karibu sana na barabara. Pia huduma za benki na posta zipo karibu na shule.

***E. Wanafunzi wanatakiwa kuja na bima ya afya ya NHIF, Aidha gharama za matibabu kwa wanafunzi zitakuwa ni jukumu la mzazi kwa kipindi chote atakachokuwa shuleni kama hatokuwa na bima.***

(Mzazi/mlezi zingatia.)

**F. MAHITAJI YA KULETA SHULENI KWA WASICHANA.**

**1) SARE YA SHULE**

Kila mwanafunzi anatakiwa kuja na sare ya shule iliyoshonwa vizuri kwa maadili ya mwanafunzi awapo shuleni. Nguo za kubana na fupi ni marufuku; na mwanafunzi hatapokelewa. Picha ya mshono wa sare ya shule imeambatanishwa.

- Sketi mbili (02) rangi kijani kibichi inayozidi magoti kwa urefu hadi kufikia kifundo cha miguu.
- Shati mbili (2) za pamba (cotton) nyeupe mikono mirefu
- Aje na tai(2) ndefu rangi ya sketi zenye miraba mieupe
- Soksi nyeupe ndefu jozi (2) au zaidi (stocking)
- viatu vyeusi vya kamba jozi (2) visivyo na visigino virefu
- Nguo za kazi shamba dress ni gauni la draft rangi ya kijani kibichi liwe na rinda box (aje nazo 2) pamoja na suruali nyeusi yenye elastic kiuononi
- Mwanafunzi aje na tranka la chuma kwa ajili ya kutunzia vifaa vyake (**mabegi ya nguo hayaruhusiwi)** mzazi/mlezi zingatia
- Mwanafunzi aje na saa ya mkononi, tochi/taa ya solar na mwavuli kwa ajili ya kujikinga na mvua.
- Kwa wasichana waislamu wanaruhusiwa kuvaa HIJABU nyeupe ifunike kifua cha mwanafunzi, iwe ndefu inayofika kwenye kifundo cha mkono mwanafunzi anaposimama; na HIJABU nyeusi kwa ajili ya kushindia.
- Mwanafunzi aje na Sweta ya Shule Nzito Rangi kijani kibichi yenye shingo ya "V"(inashauriwa mwanafunzi kuwa na sweta mbili).
- Aidha kwa wenye changamoto ya kifua waje na pullneck nyeusi (1) isiyokua na urembo.
- Aje na godoro lenye upana wa futi 2.5 na urefu wa futi 6.
- Aje na ndoo ndogo mbili za plastiki ujazo wa lita 10 kwa ajili ya matumizi binafsi ikiwemo kufulia na kuogea
- Aje na Squeezer moja na soft broom moja.
- Tisheti 2 za rangi ya kijivu zenye kola, zisizo na maandishi yeyote (nembo utapigiwa shuleni) aidha ili kuepuka kutofautiana tisheti zinapatikana duka la shule.
- mashuka mawili rangi ya pink na blanket lisilozidi kg 10
- pazia moja lenye rangi ya pink urefu wa mita (2) na upana wa mita (2)

- rangi ya kubadili rangi ya viatu (DYE) hairusiwi-tafadhali zingatia
- kandambili jozi (2)

## G. MAHITAJI YA KULETA SHULENI KWA WAVULANA.

### 2) SARE YA SHULE

Kila mwanafunzi anatakiwa kuja na sare ya shule iliyoshonwa vizuri kwa maadili ya mwanafunzi awapo shuleni. Picha ya mshono wa sare ya shule imeambatanishwa.

- Suruali (02) rangi kijani kibichi
- Shati mbili (2) za pamba (cotton) nyeupe mikono mirefu
- Aje na tai (2) ndefu rangi ya surual zenye miraba mieupe
- Soksi nyeusi ndefu jozi 2 au zaidi,
- viatu vyeusi vya kamba jozi (2) visivyo na visigino virefu
- Mwanafunzi aje na tranka la chuma kwa ajili ya kutunzia vifaa vyake, (**mabegi ya nguo hayaruhusiwi)** mzazi/mlezi zingatia
- Mwanafunzi aje na saa ya mkononi, tochi/ taa ya solar na mwavuli kwa ajili ya kujikinga na mvua.
- Mwanafunzi aje na Sweta ya Shule Nzito Rangi kijani kibichi yenye shingo ya "V"(inashauriwa mwanafunzi kuwa na sweta mbili).
- Aidha kwenye changamoto ya kifua waje na pullneck nyeusi (1) isiyokua na urembo
- Aje na godoro lenye upana wa futi 2.5 na urefu wa futi 6.
- shuka (2) zenye rangi ya blue bahari, blanketi (1) lisilozidi uzito wa kg 10
- Aje na ndoo ndogo mbili za plastiki ujazo wa lita 10 kwa ajili ya matumizi binasfsi iliwemo kufulia na kuogea.
- Aje na Squeezer moja na soft broom moja.
- Tisheti 2 za rangi ya kijivu zenye kola, zisizo na maandishi yeyote (nembo utapigiwa shuleni) ili kuepuka kutofautiana tisheti zinapatikana duka la shule
- suruali nyeusi (1) ya kitambaa(cotton) kwa ajili ya kushindia
- pazia moja rangi ya blue bahari lenye urefu wa mita (2) na upana wa mita (2)
- rangi ya kubadiri rangi ya viatu (DYE) HAIRUHUSIWI, tafadhali zingatia
- kandambili jozi (2)

**NB: VIFAA VYA VINGINE**

i) mwanafunzi aje na container, kijiko kwa ajili ya uji na chakula
ii) Baadhi ya vifaa vilivyooredheshwa hapo juu vinapatikana katika duka la shule (kalamu, penseli, rula, vijiko, sahani, vikombe, daftari, na tai )
iii) Mwanafunzi aje akiwa amevaa sare ya shule siku ya kuripoti shule.
iv) Wasichana hawatarusiwa kusuka nywele wakati wote wakiwa shuleni. Wakati wawapo shuleni nywele zinatakiwa kuwa fupi chini ya sentimita moja.

### 3) SARE ZA MICHEZO;

i. Track suit 1yenye kofia light green yenye mistari meupe pembeni isiyobana chini
ii. Tisheti rangi ya blue masai isiyo kuwa na maandishi yoyote na yenye shingo la duara (isiwe na kola)
iii. Raba / viatu vya michezo rangi nyeusi

## H. VIFAA VYA MASOMO

i. Madaftari makubwa saba (Q3) au (Q4)

ii. Kalamu
iii. Penseli
iv. Mathematical set
v. Scientific calculator (Non programmable)
vi. Graph paper
vii. Vitabu binafsi angalau kitabu kimoja kwa kila somo katika tahasusi anayosoma.
viii. Karatasi nyeupe A4 Ream 02 kwa mwaka.
ix. Nakala ya matokeo ya kidato cha nne (result slip)
x. Nakala ya cheti cha kuhitimu kidato cha nne (Leaving certificate)
xi. Nakala ya cheti cha kuzaliwa (Birth certificate)
xii. Madaftari madogo saba kwa ajili ya mazoezi ya kila siku darasani
xiii. Picha za passport size nne, ziwe zimepigwa na shati jeupe.
xiv. Rula

**I. VITABU VYA ZIADA AMBAVYO UNAWEZA KUMPATIA MWANAO .**

i) Human and Economic Geography by Gohcheug Leong, Gilliam C. Morgaw
ii) Geography An Intergrated Approach by David Waugh.
iii) Principle of Physical Geography by F.J Monkhouse.
iv) Practical Geography for Africa By John M Prichard.
v) Geography for secondary schools form five by Tanzania instituate of Education.

**ECONOMICS**

i) Modern Economics by Robert Mudida
ii) Modern Economics Theory by Dr Dewett
iii) Advanced level basic Ecomics, Mtaebwa (2012) Kampala EAP

**MATHEMATICS**

i) Advanced level pure mathematics fourth Edition by C. J. Tranter.
ii) Pure mathematics 1 by J.K Backhouse etal
iii) Pure mathematics 2 by J.K Backhouse etal
iv) Understanding pure Mathematics by A. J. Sedler and D.W. S Thoming
v) Engineering Mathematics for B.E, A. M.I.E Diploma and Non diploma stream by S. Chand

**GENERAL STUDIES**

-General studies revised version KAMILI (2017) KAMILI BOOKS AND GENERAL SUPPLIES

J. **VIFAA VYA VINGINE**

i. Sahani ya bati (stanless steel) kijiko, kikombe cha uji. (Kiwe cha chuma)

***NB:***

i. Baadhi ya vifaa vilivyooredheshwa hapo juu vinapatikana katika duka la shule (kalamu, penseli, rula, vijiko, sahani, vikombe, daftari, na tai )
ii. Mwanafunzi aje akiwa amevaa sare ya shule siku ya kuripoti shuleni.
iii. Wasichana hawatarusiwa kusuka nywele wakati wote wakiwa shuleni. Wakati wawapo shuleni nywele zinatakiwa kuwa fupi.

**K. FOMU MBALIMBALI KWA MZAZI NA MWANAFUNZI ZA KUJAZA**

Fomu mbalimbali za kujaza kwa mzazi na mwanafunzi zimeambatanishwa

**L. SHERIA, KANUNI NA TARATIBU ZA SHULE ZIMEAMBATANISHWA**

***Mwanao azisome vizuri na kuzielewa na awe tayari kufuata maelekezo na taratibu nyingine za shule.***

**M. MICHANGO YA SHULE**

***a) Mchango wa uendeshaji wa shule shilingi 65,000/=***
***b) Tahadhari Tsh 5,000/=***
***c) Nembo 5,000/=***
***d)Kitambulisho cha shule Tshs. 5,000/=***
***JUMLA YA MICHANGO NI Tshs. 80,000/=***
***Michango tajwa hapo juu ilipwe kwenye akaunti ya shule.***
***Akaunti namba 40401100047 (NMB) yenye jina KENI SECONDARY SCHOOL.***
***Baada ya malipo mwanafunzi aje na Bank pay slip siku ya kuripoti shuleni.***

**Mwisho tunamtakia mwanao safari njema ya kuja hapa Shule ya Sekondari Keni**

**………………………**
**R. LYIMO**
**MKUU WA SHULE**

***NB: Mzazi / mlezi tunaomba uthibitishe mwanao kujiunga na shule yetu mara tu upatapo nafasi ya uchaguzi wa serikali wakati ukiendelea na maandalizi mengine kwa namba 0755 642415 (Mkuu wa shule) au 0768651099/0622109659 (Makamu mkuu wa shule). Kwa changamoto yeyote itakayojitokeza tafadhali wasiliana na uongozi wa shule.***

**KIAMBATANISHO Na. 1**
**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**
**SHERIA ZA SEKONDARI………………………… (TANZANIA)**

1. **HESHIMA NA UTII**
    i. Ni lazima kila mwanafunzi atii viongozi wote kuanzia walimu, wafanyakazi, viranja na wale wote waliomzidi umri.
    ii. Ni lazima kila mwanafunzi asimame na kusalimu viongozi na wakuu wote na wote waliomzidi umri.
    iii. Ni lazima kila mwanafunzi aitike mara moja na kukimbilia mahali anapoitwa wakati asikiapo kengele au wito mwingine wowote.
    iv. Ni lazima kila mwanafunzi atii maagizo kwanza kabla ya kujenga hoja.

2. **MAHUDHURIO NA KUWAHI**
    i. Ni lazima kila mwanafunzi awapo shuleni muda wote anaotakiwa.
    ii. Ni lazima kila mwanafunzi ahudhurie na kushiriki katika vipindi vyote ndani na nje ya darasa.
    iii. Iwapo mwanafunzi ameshauriwa kutofanya kazi Fulani kwa sababu za kiafya, UTHIBITISHO wa Daktari wa Hospitali ya Serikali utahitajika.
    iv. **Mwanafunzi akikosa shule kwa zaidi ya siku tatu (3) mfululizo muhula mmoja bila sababu zenye kukubalika na shule atachukuliwa hatua za kinidhamu ikiwa ni pamoja na kusimamishwa masomo**.

3. **UVAAJI WA SARE ZA SHULE**
    i. Ni lazima kila mwanafunzi awe msafi wa mwili na mavazi.
    ii. Sare ya shule ni lazima ivaliwe wakati wote mwanafunzi awapo shuleni na wakati wowote atakapohitajika kuvaa akiwa nje ya shule.
    iii. Mashati na blauzi ni lazima yachomekwe, vishikizo vyote viwepo na kufungwa. Nywele ziwe fupi na zilizochanwa na nadhifu.
    ***N.B. Ukiukwaji wa uvaaji wa sare za shule utasababisha mwanafunzi apewe adhabu kali ikiwa ni pamoja na kurudishwa nyumbani.***

4. **MWANAFUNZI HARUHUSIWI**
    i. Kuwa na kucha ndefu
    ii. Kupaka nywele au macho au modomo rangi
    iii. Kukaanga nywele (kuweka nywele dawa)
    iv. Kuvaa kilemba, kofia, herein, mkufu, vipuli, Pete na mapambo mengine mbalimbali.
    v. Mwanafunzi haruhusiwi kutumia simu ya mtu yoyote isipokuwa itakayoelekezwa na uongozi wa shule vinginevyo akibainika hatua za kinidhamu zitachukuliwa ikiwa ni pamoja na kurudishwa nyumbani.
    vi. Kuvaa mavazi yasiyo ya heshima kama vile mini sketi, kaputla.
    vii. Kunyoa kipara, panki au kiduku.
    viii. Kufuga nywele ndefu au kusuka
    ix. Kuwa na begi la nguo

**5. LUGHA YA MAWASILIANO**

i. Lugha ya mawasiliano shuleni ni Kiingereza tu isipokuwa kwenye somo la Kiswahili na dini ikibidi wanafunzi watawasiliana na watu wengine kwa lugha ya Kiswahili ikibidi.
ii. **Ni MARUFUKU** kwa mwanafunzi kuwasiliana kwa lugha nyingine yoyote
iii. Lugha chafu ya matusi **HAIRUHUSIWI** Shuleni.

**6. USAFI WA MAZINGIRA**

i. Ni wajibu wa kila mwanafunzi kuweka eneo la shule na majengo ya shule katika hali safi.
ii. Vyoo na ukumbi wa chakula ni lazima view safi na vitumiwe ipasavyo
iii. Uchafu / takataka ni lazima zitupwe jalalani.

**7. KUTOKA NJE MIPIKA YA SHULE**

Ni Marufuku Kwa mwanafunzi kutoka nje ya mipaka ya shule wakati wa masomo au kazi nyingine nje ya darasa bila ruhusa. Ruhusa itatolowa na mwalimu wa zamu na kuidhinishwa na mkuu wa shule au makamu wa shule na kupewa kibali maalumu (permission slip) na mara arudipo akirudishe kibali kwa mwalimu wa zamu.

Mwanafunzi awapo shuleni ni marufuku kutembelea sehemu zifuatazo bila sababu maalumu.

i. Chumba cha walimu (staff – room)
ii. Nyumba za walimu na watumishi wasio walimu.
iii. Ofisi na stoo za shule.
iv. Jikoni.
v. Karakana na maabara.
vi. Sehemu zenye mashamba na mifugo.

**8. MICHEZO**

Ni lazima kila mwanafunzi ashiriki katika michezo inayofanyika shuleni. Hivyo awe na nguo za michezo kama viatu (raba), T- Shirt au "Truck Suit". Kwa wale wenye changamoto za kiafya waje na maelezo ya daktari.

**9. ADHABU ZINAZOTOLEWA NA SHULE**

i. Kuonywa kwa mdomo na maandishi.
ii. Kurudishwa nyumbani kwa muda ama kufukuzwa shule.
iii. Kufanya kazi za nje.
iv. Kufikishwa katika kamati ya nidhamu kwa hatua kali za kinidhamu.#
v. Kuchapwa viboko.

**10. MAKOSA YA KUFUKUZWA SHULE**

i. Wizi
ii. Ulevi na pombe au madawa ya kulevya.
iii. Uvutaji bagi / sigara.
iv. Kuanzisha au kushiriki katika mgomo au fujo za aina yoyote shuleni.
v. Kutoheshimu alama za Taifa kama vile Bendera ya Taifa, Picha ra Rais ya Jamuhi wa Muungo wa Tanzania na makamu wake, Fedha ya Tanzania n.k
vi. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
vii. Uasherati.
viii. Kupata mamba au kutoa mamba.

ix. Kuolewa
x. Kukataa adhabu iliyotolewa na uongozi wa shule
xi. Kupigana ua kumshambulia mtu yeyote au kuzomea au lugha ya matusi.
xii. Kutohudhuria masomo.
xiii. Utoro wa vipindi wa muda mrefu
xiv. Kukataa kufanya usafi wa maeneo shuleni
xv. Mwanafunzi kuwa na simu ya mkononi
xvi. Mwanafunzi kuwa na radio shuleni. Vyombo vya habari vipo shuleni eg. TV
xvii. Kuwa na pasi shuleni.
xviii. Kuwa na manukato (spray, perfume na lotion zenye harufu kali)
xix. Kuchubua ngozi.

***N.B: Mzazi / mlezi utalazimika kufika shuleni pindi mwanao abainikapo kuwa na makosa hayo na utaondoka naye kwenda nyumbani***

**(KIAMBATANISHO NA. 2)**
**KANUNI NA TARATIBU ZA SHULE**
**WAJIBU WA MWANAFUNZI ANAYESOMA SHULE YA SEKONDARI**

Mwanafunzi yeyote anatakiwa afahamu, azingatie na afuate taratibu zifuatazo.

1. Kuwa na heshima kwa walimu, watumishi wengine na wote waliomzidi umri na wadogo.
2. Kuongea lugha safi isiyo na matusi wala kushfa kwa binadamu yeyote awaye.
3. Kushiriki na kusaidiana katika kazi za shule.
4. Kuwahi shule, kufanya kazi zote za shule kuendana na maagizo yatolewayo na uongozi wa shule.
5. Kuhakikisha kwamba mazingira ya shule anakoishi yanakuwa safi wakati wote, kwa kufanya usafi.
6. Kusimama na kusalimia wakubwa wanapopita mbele yake na walimu wanapoingia darasani.
7. Kupokea kwa heshima mizigo kwa watumishi wa shule na wageni wa shule na kuwasaidia.
8. Kuheshimu bendera ya Taifa, wimbo wa Taifa, wimbo wa shule Nembo za Taifa, Fedha za Taifa, Picha za viongozi wa serikali. nk.
9. Kutii na kuheshimu wito wowote unaotolewa shuleni na kengele inapopigwa.
10. Kutii na kuheshimu wito na kengele mara tu inapogongwa.
11. Kuheshimu mahali pa mikusanyiko kwa utulivu, na kufuata utaratibu uliowekwa.
12. Kuheshimu na kutunza mali za umma na binafsi.
13. Kusoma kwa bidii na kufanya mazoezi ya mitihani yote inayotolewa na Taifa.
14. Kufuata sheria zote za shule
15. Kuwa mzalendo Kwa mambo yote yanayohusu shule, jamii na Taifa.

***FOMU B***

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA ELIMU SAYANSI TEKNOLOJIA NA UFUNDI**

**SHULE YA SEKONDARI KENI**,
S. L. P. 144,
**MKUU – ROMBO.**

8/7/2024.

**FOMU YA MAPOKEZI SHULENI – MAELEZO KUHUSU MWANAFUNZI**

**SEHEMU A: (Ijazwe na mwanafunzi)**

1. Jina la mwanafunzi (majina matatu)..............................................................................
2. Taifa ...........................................................................................................................
3. Tarehe ya kuzaliwa.........................................................................................................
4. Dini..............................................................................................................................
5. Shule anayotoka.............................................................................................................
6. Tarehe ya kutoka Shule...................................................................................................

**SEHEMU B: (Ijazwe na mzazi / mlezi)**

1. Jina la mzazi / mlezi (majina matatu)...............................................................................
2. Mahali unapoishi Kata...................................................Kijiji.........................................
3. Anuani ya mzazi / mlezi...........................................Namba ya simu............................
4. Kazi ya mzazi / mlezi..................................................Mahali anapofanya kazi na amwani...................................................................................

Ndugu wawili wa karibu (unaowaelewa badala ya mzazi/ mlezi)

a. Jina .........................................................................................
   Anwani.......................................................................................
   Simu namba.................................................................................
   Uhusiano wake na mzazi / mlezi.....................................................
b. Jina.........................................................................................
   Anwani.......................................................................................
   Simu namba.................................................................................
   Uhusiano wake na mzazi/ mlezi......................................................
   Jina la mzazi / mlezi .........................................................................
   Tarehe.......................................................................................
   Sahihi.......................................................................................

**(KIAMBATANISHO Na 3)**

**MKATABA NA KAULI YA KUKUBALI KUTII SHERIA, KANUNI NA TARATIBU ZA SHULE**

Mimi…………………………………………………………………………………… (Jina la mwanafunzi)
Ninakiri kuwa nimesoma na kuzielewa vizuri sheria, kanuni na taratibu za shule kama zilivyoainishwa katika vipengele vyote, na kuwa mara nikiukapo sheria hizo hatua za kinidhamu zichukuliwe kama zilivyoainishwa dhidi yangu.

JINA LA MWANAFUNZI………………………………………………………………………………
SAHIHI YA MWANAFUNZI…………………………………………………………………………….
TAREHE………………………………………………………………………………………………

Mimi……………………………………………………………..(Mzazi / mlezi wa mwanafunzi) wa mwanafunzi……………………………………………(Jina la mwanafunzi) wa kidato cha……………..
tahasusi (comb) ya ………………………………..
Nakiri kupokea kusoma na kuzielewa taratibu zote zilizo kwenye maagizo ya kujiunga na shule ya sekondari ya Keni. Iwapo mwanangu atakiuka taratibu hizo nitakuwa tayari kukubali hatua zitakazochukuliwa dhidi yake na shule. Nitakamilisha mahitaji yote ya shule kwa wakati.

JINA LA MZAZI / MLEZI ………………………………………………….
Namba za simu…………………………………………………………..
SAHIHI YA MZAZI / MLEZI……………………………………………
TAREHE…………………………………………………………………
Namba ya simu ya ndugu/ Jamaa wa karibu…………………………………..

***FOMU C***

**PRESIDENT'S OFFICE REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**
**ROMBO DISTRICT COUNCIL**
**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

**Keni Secondary School**
**P. O. Box 144, Mkuu - Rombo**
**Mobile 0752106188**

## MEDICAL EXAMINATION FORM

### PART I: PERSONAL PARTICULARS (To be filled by the candidate)

Surname...............................................Other names...............................................
Age................ Sex...............Combination........................School.............................................

PART II: PERSONAL HISTORY (To be filled by medically qualified and registered professional)

Are your suffering of have you suffered from any of the following? indicate Yes or No

1. Tuberculosis..............................................Epilepsy....................................
2. Asthma............................................Deformity...........................................
3. Rheumatic fever.......................................Mental illness...............................
4. Allergic disorders...................................... Eye disorder....................................
5. Heart disease ........................................Ear, Nose, Throat disorder.........................
6. Gastric or duodenal ulcers.........................Skin disease............................
7. Jaundice................................ Anemia.................................
8. Dysentery................................ Varicose veins.............................
9. Kidney disease ..........................Diabetes.....................................
10. Gynecological disorder ........................... Any other serious disorder (specify)

### PART III: PHISICAL EXAMINATION

1. Height (cm)...................................
2. Skin.................................................
3. Weight (kg)........................................
4. Eyes: Conjunctive.................................Pupil...........................Vision
   Right..........................................Left..........................
5. Ears (state if any discharge)................................Mouth / throat ..........................
6. Nose ..................................Respiratory system....................................
7. Abdomen..............................Any abnormality...............................
8. Cardiovascular system..........................Blood pressure..........................
   Systolic......................................Diastolic..................................
   Heart: Any murmur....................................Arteries veins...............................

### PART IV: LABORATORY

1. Urine: Albumin................................Sugar........................Leucocytes.......................
   Schistosoma................................
2. Stool: Special emphasis on hookworms or schistosoma................................
3. Blood examination
   a. Hb level...........................................................
   b. Neutrophil..........................................................
   c. Eosinophils.............................................................
   d. Basophiles..................................................
   e. Lymphocytes...................................................
   f. Monocytes......................................................
   g. ESR..............................................................

4. X- ray examination: Chest (include Radiologist's report)...............................................
5. Serology widal test.......................................VDRL........................................................
6. Pregnacy test.....................................

## PART V: CONCLUSION

I have examined miss.................................................and consider that she is physically and mentally fit/ not to be admitted for secondary education.

Name................................................. Title.......................
Qualification............................................ Signature .................................Date...................
Address ......................................
.........................................................
.........................................................

*DESIGNATION/ STAMP…………………………………..*

*DATE…………………………………………………………*

*STATION……………………………………………….*